

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI**



TAARIFA KWA UMMA

**KUKANUSHA TAARIFA ILIYOTOLEWA NA GAZETI LA
MTANZANIA LA TAREHE 27 FEBRUARI, 2010**

Katika gazeti la Mtanzania la tarehe 27 Februari, 2010, ukurasa wa mbele, liliandika taarifa kwamba "Katibu Mkuu adanganya Bunge" iliyoandikwa na Primitiva Pancras ambaye ameuzelea umma kupitia gazeti hilo kwamba Naibu Katibu Mkuu John Haule alitoa taarifa zenye utata mbele ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu wizi wa mishahara ya walimu ya Tshs. Bilioni 8.3, ambapo kamati hiyo iliambiwa kwamba tayari wahusika wameburuzwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati hakuna kesi ya aina hiyo katika Ofisi za Mkurugenzi wa mashtaka nchini (DPP) wala katika mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu – Dar es Salaam.

Wizara ya Fedha na Uchumi inapenda kukanusha taarifa iliyotolewa katika gazeti hilo. Taarifa hiyo siyo sahihi na imepotosha umma. Ukweli ni kwamba, Naibu Katibu Mkuu Bw. John Haule, mbele ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, alielezea kuhusu hoja ya ukaguzi ya mwaka 2001/02 ya upotevu wa fedha za mishahara kiasi cha Sh.8.3 bilioni unaohusisha waliokuwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa 63 nchini pamoja na baadhi ya Wafanyakazi wa Serikali Kuu. Aidha alielezea Kamati hiyo kuwa kutokana na upotevu huo kulikuwa na Kesi mbalimbali zilizofunguliwa katika Mahakama za Mikoa ambazo zilihusu watumishi waliotuhumiwa kutoka Halmashauri za Serikali za Mitaa

na kwa hapa Dar es Salaam Kesi inayohusika ni ECC Na. 8 ya mwaka 2005 iliyofunguliwa katika Mahakama ya Hakim Mkazi Kisutu ambaye inahusisha baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu. Iliarifiwa kuwa Kesi hiyo ingetajwa tarehe 18 Januari, 2010 na ingeendelea kusikilizwa tarehe 2 Februari, 2010. Kwa taarifa, Kesi hiyo inasimamiwa na kuendeshwa chini ya Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU). Kwa msingi huo tunapenda kumweleza Primitiva Pancras na uongozi wa gazeti la Mtanzania kwamba kesi hiyo haiendeshwi na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), bali inaendeshwa na TAKUKURU.

Aidha kesi hiyo kwa sasa itaendelea kusikilizwa katika Mahakama ya Hakim Mkazi Kisutu katika tarehe itakayopangwa ambapo mashahidi wa upande wa Serikali wataendelea kutoa ushahidi wao.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, Wizara ya Fedha na Uchumi inapenda kuarifu umma na kulihakikishia Bunge kuwa taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati yake ya Hesabu za Serikali ni sahihi. Hivyo kutokana na upotoshaji uliojitokeza, Wizara ya Fedha na Uchumi inawataka Viongozi na Mhariri wa gazeti la Mtanzania kukanusha taarifa iliyotolewa katika gazeti hilo la tarehe 27 Februari, 2010 kupitia ukurasa wa mbele na vilevile waitake radhi Wizara ya Fedha na Uchumi kwa taarifa hiyo potofu. Ni muhimu kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari kuhakikisha kuwa wanatoa taarifa zilizohakikiwa ipasavyo na ni sahihi ili kuepuka hali kama hii kujitokeza.

Imetolewa na



Ramadhani M. Khijjah

KATIBU MKUU

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

3 Machi, 2010